Kioo cha Lugha
Juzuu 1, Na. 1 (1995)

# UAMBAJENGO WA VIULIZI KATIKA KISWAHILI

Z.S.M.Mochiwa
Idara ya Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

## 1.0 Utangulizi

Katika kila lugha kuna aina kadhaa za maneno ambayo kwayo wasemaji huwakia virai vya aina kadhaa. Virai hivyo ndivyo vinavyowapatia wazungumzaji wa lugha uwezo na kuunda sentensi kadhaa wa kadha, na hata kuzitumia sentensi hizo kuundia sentensi nyingine thakili zaidi. Tabia hii ya kuingizika kwa maneno katika vitengo ndio mwega wa ufunzikaji wa lugha yoyote. Kwa hiyo inamkinika kukaza hoja kuwa kazi moja ya mtu anayejifunza lugha ni kubainisha maneno na kufichua uambajengo wake. Katika hima hiyo jitihadi inayofanyika ni ya kutafuta kila neno linaingia katika kiambajengo cha aina gani. Hivi ni kusema swali kuu la kwanza la kisintaksia ambalo mtu anayejifunza lugha inayohusika hujiuliza ni hili: Neno **X** ni sehemu ya kirai gani? Hali kadhalika mtu huyo atajiuliza tena: Katika kirai hicho hili neno **X** lina dhima gani kisintaksia? Mara baada ya kupata majibu ya maswali hayo mtu huyo atakuwa amepata uwezo wa kutafuta namna ya kuvitumia viambajengo hivi vikubwa katika kuwaka viambajengo vikubwa zaidi yaani sentensi za lugha.

Katika makala hii fupi tunamakinikia maswali mawili ya kwanza. Tunakusudia kudadisi uambajengo wa viulizi katika kiwango cha virai. Tutadadisi mienendo ya kisintaksia ya viulizi **nani, gani, nini, wapi, vipi**. Hususan udadisi huu unakusudiwa kutafuta majibu ya maswali mawili makubwa: (a) Katika mawako, viambajengo gani huchukua viulizi? (b) Katika uambajengo huo, viulizi vina dhima gani kisarufi? Katika kufanya hivyo, tutaonesha viulizi vinaingia katika virai gani na halafu tutajaribu kuukilia dhima ya kisintaksia ya kila kiulizi ndani ya kirai chake.

## 2.0 Uchambuzi

Maneno ya Kiswahili yamegawanyika katika aina nane: nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi, kihusishi kiunganishi, kiingizi, kiwakilishi. Katika kiwango cha juu zaidi, kuna kirai - nomino, kirai-kitenzi, kirai-kivumishi, kirai-vielezi n.k. kutegemea kama katika kirai kinachohusika, nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi n.k. ndicho kipashio kikuu. Kwa ukuu wake kwa mfano nomino inaweza kuwa peke yake katika kirai na bado ikahesabika kuwa inajenga kirai kinachohusika kwa kuwa nomino hiyo huweza kurithiana na kirai-nomino kingine katika utungo pasipo mparaganyo wa kisarufi. Mfano huu ufuatao unadhihirisha hoja hii:

(1) **Watoto wawili wakubwa** wamelala

Sehemu ya sentensi (1) iliyoandikwa kwa herufi nzito huweza kurithiwa na kipashio kimoja tu kama **watu, wanafunzi, wakulima,** na ke bado sentensi hiyo ina virai viwili: kirai-nomino na kirai kitenzi. Aidha hiki kirai cha pili kina kipashio kimoja tu: **Wamelala.** Inawezekana, kwa mfano, kupata kirai-kitenzi chenye vipashio vingi kama inavyoonekana katika (2) hapa chini:

(2) Watoto wawili wakubwa **wamenunua machungwa mane**

Pengine inafaa idokezwe kuwa nomino na vivumishi vina mahusiano ya karibu kisintaksia (Taz. Sells 1985,Radford 1981). Hali hii huvipa vivumishi uwezo wa kuchukua makamu ya kurithiana na nomino zilizomo ndani ya kirai kimoja. Kwa msingi huu utungo huu (3) unakubalika kwa kutegemea mazingira.

(3) Wawili wamenunua mane

Ingawa swala hili litajadiliwa kwa undani zaidi baadaye lakini itafaa tutaje kwamba mfumo wa upatanisho wa kisarufi - angaa katika Kiswahiuli - husuhulisha utaratibu huu kwa kiasi kikubwa. Kwa kuwa jitihadi ya kudadisi mienendo ya kisintaksia ya viulizi inajikita katika kufichua viambajengo vinavyovichukua tutaanza udadisi wetu kwa kutoa nadharia - tete ya kwanza inayodai kuwa viulizi ni sehemu ya virai-nomino.

## 3.1. Uambajengo wa Viulizi

Katika kuudadisi ukweli wa nadharia-tete hii tuangalie data hii ifuatayo:

(4) (a) Walimu wananunua **nini?**
(b) **Nani** wananunua machungwa mawili?
(c) Walimu **gani** wananunua machungwa mawili
(d) Walimu wananunua machungwa mawili **yapi?**
(e) Mwalimu **yupi** ananunua machungwa mawili
(f) Walimu wananunua machungwa mawili vipi?


Maswali yote haya - isipokuwa (4f) - yana mawako yanayolingana. Dai hili huthibitishika kwa njia mbili. Kwanza katika kuyajibu maswali haya ni lazima yatumike maneno ya aina ambayo kwa desturi huingia ndani ya kirai-nomino. Tuangalie majibu hayo katika setiya data ifuatayo:

(5) (a) Walimu wanaunua **machungwa mawili**
(b) **Walimu** wananunua machungwa mawili
(c) **Walimu wanene** wananunua machungwa mawili
(d) Walimu wananunua machungwa mawili **haya**
(e) Mwalimu **huyu** ananunua machungwa mawili
(f) Walimu wananunua machungwa mawili **kwa mkopo**

Kwa kuangalia data ya maswali (4) na ya majibu (5) tunaona kuwa:

| | | |
|---|---|---|
| **nini** | imerithiwa na | **machungwa mawili** |
| nani | " | " walimu |
| gani | " | " wanene |
| yapi | " | " haya |
| yupi | " | " huyu |
| vipi | " | " kwa mkopo |

Pili kutokana na mahusiano haya ya urithiano, inawezekana kuchora ngoe moja inayoonesha viboya vya virai kama ilivyo hapa chini.




Ukiondoa swali la (4f) maswali yote haya yanaonesha kuwa viulizi vyake ni sehemu ya kirai-nomino ama cha kabla au baada ya kitenzi (T). Hata hivyo inafaa ikumbukwe kuwa virai-nomino vya kabla ya kitenzi (T) vya maswali mengine kama vile (4a) (4b) na (4d) vina kipashio kimoja kimoja tu.

Virai-nomino, kama virai vinginevyo, hushiriki katika kanuni mbalimbali za kisintaksia. Mathalan katika kanuni ya utendwa/utendewa virai-nomino vilivyomo katika utungo hubadilishana nafasi. Kwa kuitumia kanuni hii peke yake tutaweza kuthibitisha mambo kadhaa. Kwanza, ikiwa ni sehemu ya virai-nomino, viulizi huhama wakati virai-nomino vinashiriki katika kanuni ya utendwa/utendewa. Pili, kwa kuwa kanuni ya utendwa/utendewa hukifanya kirai-nomino kinachohamia mwishoni kutawaliwa na kihusishi, na kwa kuwa tabia moja ya kisintaksia ya kirai-nomino ni uwezo wa kutawaliwa na kihusishi, matumizi ya kanuni hii yatazidi kututhibitishia kuwamo kwa viulizi ndani ya virai-nomino. Maswali ya nambari (4) huwa katika sura hii baada ya kutumika kwa kanuni ya utendwa/utendewa.

(7)
- (a) **Nini** kinanunuliwa na walimu?
- (b) Machungwa mawili yananunuliwa na **nani?**
- (c) Machungwa mawili yananunuliwa na walimu **gani?**
- (d) Machungwa mawili **yapi** yananunuliwa na walimu?
- (e) Machungwa mawili yananunuliwa na mwalimu yupi?
- (f)* Machungwa mawili vipi yananunuliwa na walimu?
- (g) Machungwa mawili yananunuliwa na walimu vipi?

Kwa kuwa **machungwa (mawili) (yapi) na (M)walimu (gani/yupi)** ni vira-nomino katika maswali ya nambari (4), matumizi ya kanuni ya utendwa/utendewa yamevilazimisha vibadilishane nafasi kama ilivyodhihirika katika seti ya data nambari (7). Kutokubalika kwa (7f) kunaonesha kuwa kipashio **vipi** si sehemu ya kirai nomino. Aidha kwa sababu hii kuachwa kwake kumefanya (7g) ikubalike.

Kwa bahati mbaya hatutajadili hadhi ya kisintaksia ya kipashio **vipi.** Muhimu kwetu ni ule ukweli kwamba ingawa viulizi vingi huwa sehemu ya kirai-nomino, kuna vingine, kama **vipi** viko nje ya virai-nomino.

Kwa ajili ya kuthibitisha zaidi kuwa viulizi hivi vyote vinaingia katika kirai-nomino isipokuwa **vipi** tutatumia kigezo kingine cha sentensi ya `klefu' (cleft sentence). Mawako ya utungo wa klefu ni haya:

Ni X + S[+ Urejeshi]

ambapo X ni kirai nomino. Ikiwa kiulizi ni sehemu ya X, basi kinaweza kutokea kabla ya sentensi yenye urejeshi. Kwamba viulizi hivyo vimo katika kirai-nomino huthibitika kwa kukubalika kwa tungo zifuatazo.

(8) (a) Ni **nini** wanachonunua walimu?
(b) Ni **nani** wanaonunua machungwa mawili?
(c) Ni **walimu gani** wanaonunua machungwa mawili?
(d) Ni **machungwa mawili yapi** walimu wanayonunua?
(e) Ni **mwalimu yupi** anayenunua machungwa mawili?

Kigezo hiki nacho kinaonesha kuwa vielezi **nini, nani, gani, yapi** na **yupi** vinaingia katika kirai nomino kama **machungwa** katika **machungwa mawili** na watoto katika **watoto wazuri** zilivyo sehemu ya kirai-nomino katika sentensi hizi za klefu.

(9) (a) Ni machungwa mawili ninayotaka
(b) Ni watoto wazuri waliopotea.

Unapotumika katika utungo wenye kiulizi **vipi** utaratibu huu huu unatupatia utungo uliopogoka kisarufi.

(10) *Ni machungwa mawili vipi walimu wanayonunua?

Hii inazidi kutupatia ushahidi wa kukazia hoja yetu kuwa kiulizi **vipi,** kama kilivyotumika katika (7f) si sehemu ya kirai-nomino chochote.

Mpaka hatua hii tumepata ushahidi wa kutosha kwa kukazia hoja yetu kuwa viulizi **gani, ngapi, yupi, nani,** na **nini** huingia katika kirai-nomino. Inatubidi sasa tudadisi dhima za viulizi hivyo ndani ya kirai-nomino.

## 3.2. Dhima za kisarufi

Kwa desturi katika kirai-nomino hupatikana nomino ambayo ndiyo kiambajengo kikuu. Nomino hii huweza kuwa peke yake au ikawa na kivumishi chake. Pengine kivumishi nacho kinaweza kuandamana na kisisitizo chake (intensifier). Swali lililo mbele yetu sasa ni kudadisi kama viulizi ni nomino au vivumishi. Ikiwa viulizi ni nomino vitakuwa na mwenendo wa nomino kisintaksia. Kwa mujibu huo viulizi vitakuwa na uwezo wa kukubali vivumishi. Sasa tuichungue data ifuatayo:

(11) (a)? **Nani wazuri** wamepotea?
(b)? **Nini vizuri** vimepotea?
(c)* **Gani wembamba** wamepotea?
(d) **Wangapi wembamba** wamepotea?

Data hii inatupatia matokeo yaliyochanganyika. **Nani** na **nini** huonesha kuwa vina walakini ambao unavumilika lakini **gani** imekataliwa kabisa. Kwa mujibu wa Kiswahili cha mchambuzi, **wangapi**, kama ilivyotumika katika (11d), haina dosari. Matokeo haya yanaelezekaje? Kuvumilika kwa **nani** na **nini** kunadhihirisha kuwa viulizi viwili hivi viko karibu sana na nomino. Viulizi hivi, hitilafu na **gani**, vinaweza kushika makamo ya nomino. Katika lugha, vipashio vyenye uwezo huo ni viwakilishi kama **mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi, wao, n.k.** Hapana shaka kuwa **nani** na **nini** ni viwakilishi viulizi. Kwa tabia yake viwakilishi havikubali kuvumishwa bila ya kuwako kwa hitilafu. Ni kwa sababu hii tungo zifuatazo zinakwaruza kidogo.

(12) ? **Mimi mbaya** ninachukiza
ling. Mimi niliye mbaya ninachukiza.
? **Nyinyi wazuri** mtapata zawadi
ling. nyinyi mlio wazuri mtapata zawadi.

Mkwaruzo unaojitokeza hapa si tofauti sana na ule uliopatikana wakati viulizi nani na **nini** vilipovumishwa. Kwa msingi huu mwenendo wa kisintaksia wa viulizi hivi unalinganalingana na ule wa viwakilishi.

Kukubalika kwa (11d) **Wangapi wembamba wamepotea?** kunaonesha kuwa kiulizi **wangapi** kina mwenendo unaofanana na nomino. Kwa mwenendo huu, kiulizi hiki hakina tofauti na **wawili** au **wavivu** katika data ifuatayo:

(13) **Wawili** wembamba wamepotea.
**Wavivu** wembamba wamepotea.

Hali hii inatuletea maswali makubwa mawili: **Wangapi** ni nomino au kivumishi? **Wangapi** ni tofauti na **gani?** **Wangapi** kisingekuwa kiwakilishi kwa sababu kinakubali uvumishi bila ya hitilafu yoyote (411d). Ili kujibu maswali haya inatubidi tusuke nadharia tete ya pili. Ikiwa kimo ndani ya kirai-nomino na maadamu si nomino, kiulizi hicho kitakuwa kivumishi. Kama ni kivumishi, kiulizi hicho kitakuwa na uwezo wa kutanguliwa na nomino inayovumishwa nacho. Kwamba hivyo ndivyo ilivyo inathibitishwa na data hii ifuatayo:

(14) (a) watu gani wamepotea?
(b) watu wangapi wamepotea?
(c) *watu nani wamepotea?
(d) *vitu nini vimepotea?
(e) mtu yupi amepotea?
(f) Mahali wapi panafaa?

Kupogoka kwa (14c) na (14d) kunazidi kututhibitishia kuwa **nani** na **nini** si vivumishi na wala si nomino. Nomino inaweza kutumika katika uvumishi kama data hii inavyoonesha.

(15) (a) Kijana mwanamke amekuwa wa kwanza
(b) Mwalimu Mpare anafundisha
(c) Padre kijana anatoa misa
(d) Vijana wanawake wanafundisha.

Kushindikana kwa matumizi ya viulizi **nani** na **nini** katika uvumishi hakuna tofauti na kushindikana kwa matumizi ya viwakilishi **yeye, nyinyi** katika data hii:

(16)? Kijana yeye amekuwa wa kwanza
? Walimu nyinyi mnafundisha vizuri.

Kukubalika kwa sentensi nyingine zilizosalia katika seti ya data ya (14) kunatuthibitishia kuwa viulizi **gani, wangapi, yupi,** na **wapi** ni vivumishi. Sasa jambo la kujiuliza ni hili: **wangapi** hutofautiana vipi na **gani?** Itakumbukwa kuwa wangapi huweza kusimama peke yake bila ya nomino inayovumishwa lakini **gani** hairuhusu utaratibu huo. Tujipe wasaa mwingine wa kuuzingatia ukweli huu.

(17)* Gani watapotea?
Wangapi watapotea?

Hitilafu hizi za mwenendo zingeelezeka kwa kutumia moja ya hoja mbili hizi: Ama inaweza kudaiwa kuwa hitilafu hizo zinatokana na neno lenyewe **gani** kuwa na upekee; ama katika lugha ya Kiswahili viko vivumishi vyenye upekee fulani. Hoja hii ya pili inakolea zaidi, kwa sababu upekee wa **gani** unaonekana katika vivumishi vingine ambavyo si viulizi. Fikiria vivumishi kama **safi, ghali, rahisi,** n.k. katika tungo zifuatazo:

(18) (a) Maji safi ni adimu
ling. (b): safi ni adimu
(c) Magauni ghali ni adimu
ling. (d)? Ghali ni adimu
(e) Wafanyakazi rahisi ni adimu
ling. (f)? Rahisi ni adimu.

Mushkeli unaojitokeza katika data hii - kama upo - si mkubwa sana endapo vivumishi vitumikavyo ni kama **wazuri, virefu, madogo** n.k. kama inavyoonekana katika data ya (19).

(19) (a) Watoto wazuri ni adimu
(b) Wazuri ni adimu
(c) Vikombe virefu ni adimu
ling.(d) Virefu ni adimu
(e) Magauni madogo ni adimu
ling. (f) Madogo ni adimu.

Tofauti kati ya vivumishi hivi imo katika mofolojia ya vivumishi vyenyewe. Vivumishi vinavyojitokeza katika data ya (18) havina viambishi vya upatanishi wa kisarufi ilihali vile vilivyomo katika data ya (19) vinavyo. Tofauti hii ya kimofolojia ndiyo chimbuko la tofauti ya kisintaksia inayojitokeza baina ya vivumishi hivi. Vivumishi vinavyochukua viambishi vinaweza kudondosha nomino vinazovumisha na bado kile kiambishi kikasaidia katika uwakilishi. Vivumishi kama **ghali, gani, safi** n.k. havina uwakilishi huu na kwa sababu hii vikitokea peke yake bila ya nomino huleta mushkeli. Hivyo basi tofauti ya **gani** na viulizi vingine ambavyo ni vivumishi inatokana na **gani** kukosa hii nguvu ya uwakilishi ambao msingi wake ni upatanishi wa kisarufi.


Baada ya kudadisi mienendo ya viulizi ndani ya virai-nomino, sasa tuchungue zaidi mwenendo wa virai-nomino ambavyo vina viulizi. Katika hima hii yatafanyika mambo mawili: kwanza tutaangalia uunganishi na halafu tutaangalia uhusishi.

## 3.3 Viunganishi

Namna moja inayosaidia kuukilia uambajengo pacha wa vipashio ni matumizi ya kiunganishi. Viambajengo vinavyounganishwa hadi kukapatikana kiambajengo thakili ni vile vyenye dhima moja kisarufi. Hivyo nomino huunganishwa na nomino, kitenzi na kitenzi, kivumishi na kivumishi n.k. Aidha kwa mujibu huo kirai-nomino huunganishwa na kirai-nomino kingine. Uunganishi utatusaidia kuthibitisha zaidi unomino wa **nani** na **nini** na uvumishi wa **wangapi, gani, yupi** n.k. Tutaanza na maswali haya:

(20) (a) Nani na nani watapata zawadi?
(b) Juma na nani watapata zawadi?
(c) Nani na Juma watapata zawadi?
(d) Nani na nini vimepotea?
(e) Nini na karatasi vimepotea?
(f) Karatasi na nini vimepotea?
(g) Yupi na yupi wamepotea?
(h) Juma na (mtoto) yupi wamepotea?

Data iliyotolewa katika (20) inaonesha kuwa **nani** na **nini** huweza kuunganishwa na nomino. Mathalani **Nani na Juma** (20c) ni kirai-nomino kama kilivyo **Juma na Ali** na mawako yake huweza kuonekana katika kielelezo hiki cha mti:




Uunganishi hauwezi kutumika kwa **gani** kwa sababu ile ile ya kukosekana kwa uwakilishi. Hivi ni kusema sababu ile ile inayozuia ukabalifu wa ***Gani amepotea?** inaendelea kuzuia: **Gani na gani wamepotea.** Inapasa pia kuelezwa kuwa ingawa **Juma na nani** haina mushkeli wowote lakini **nani na Juma** ina walakini. Sababu kubwa ya hali hii ni mwelekeo wa wazungumzaji wa kuanza kutaja vijulikanavyo kabla ya vile visivyojulikana. Hivyo kwa desturi katika kirai-nomino thakili chenye uunganishi viulizi havitangulii. Hivyo kwa mfano: **kitabu na nini** hutokea zaidi kuliko **nini na kitabu.** Sasa tuangalie mwenendo wa viulizi ndani ya virai-vihusishi.

## 3.4 Uhusishi

Kama ilivyosemwa huko nyuma virai-nomino huingia katika virai-vihusishi pia. Mathalan inapotumika kanuni ya utendwa/utendewa husababisha kirai-nomino kimoja kuingia katika kirai-kihusishi. Hali kadhalika vitenzi vingine hufuatwa na virai-vihusishi badala ya virai-nomino. Data inayofuata inathibitisha dai hili.

(21) (a) Watoto wamefundishwa na nani?
(b) Kikombe kimevunjwa na nini?
(c) Mtoto amekula na nini?
(d) Wewe utakwenda na nani?
(e)* Kikombe kimevunjwa na gani?
(f) Zamu imeangukia kwa nani?

(g) Mwalimu aliondoka na vingapi?

Kupogoka kwa (21e) kunatokana na ukweli kwamba **gani** haiwezi kuwa peke yake katika kirai-nomino. Ushinde huu unatokana na kukosekana kwa uwakilishi wa nomino.

Hali kadhalika kirai - kihusishi chenye kirai-nomino chenye kiulizi huweza kutumika katika sentensi za klefu bila ya hitilafu. Tuangalie data hii.

(22)
- (a) Ni ya nani?
- (b) Ni ya nini?
- (c)* Ni ya gani?
- (d) Ni ya wapi?
- (e) Ni ya yupi?

Kama ambavyo ingetarajiwa, ***Ni ya gani?** haina ukubalifu kwa sababu **gani** peke yake haimudu kuchukua dhima ya kirai-nomino.

## 4.0 Mwisho

Katika makala hii fupi tumejaribu kuonesha kuwa viulizi vilivyo vingi vimo katika virai-nomino. Kutokana na uambajengo wake huo viulizi hivyo, ama hufanya kazi ya nomino au vivumishi. Hali kadhalika kwa kuwa ndani ya virai-nomino viulizi huathirika wakati inapotumika kanuni inayohusu virai-nomino hivyo. Mathalan viulizi vitahamishwa wakati kirai-nomino chake kinapohama. Tumezingatia kuwa hakuna viulizi ambavyo ni nomino hasa isipokuwa kuna viwakilishi. Hivi ni kusema **nani na nini** si nomino bali ni viwakilishi vya nomino. Kwa kuwa ni viwakilishi vina uwezo wa kuchukua makamu ya nomino lakini haviwezi kuvumishwa bila ya kutokea dosari. Mwenendo huu hauna tofauti sana na viwakilishi vinginevyo ambavyo si viulizi.

Imedhihirika pia kuwa viulizi ambavyo ni vivumishi hutofautiana. Kuna viulizi ambavyo huweza kuchukua makamu ya kirai-nomino na viko ambavyo haviwezi kufanya hivi. Imeelezwa kuwa kiulizi kivumishi huweza kuchukua makamu ya nomino inayovumishwa ikiwa kiulizi hicho kina uwakilishi wa nomino unaojengeka katika upatanishi wa kisarufi.

Mwisho, makala hii haikuchunguza kwa makini viulizi ambavyo haviingiii katika kirai-nomino. Kwa mfano haikufanyika jitihadi maalum katika kutafiti mwenendo wa kiulizi **vipi** isipokuwa kuonesha ile tofauti yake na hivi vingine vilivyojadiliwa. Hapana shaka kuwa hiki ni kipengee ambacho kinahitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

## MAREJEO


Akmajian, A. et al (1975) **An Introduction to Transformational Syntax.** MIT Press Cambridge. Massachussetts.

Kapinga, M.C. (1983) **Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu**. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. ChuoKikuu cha Dar es Salaam.

Radford, A. (1981) **Transformational Syntax: A Student's Guide to Chomsky's Extended Standard Theory**. C.U.P. Cambridge London.

Soames, S. and Perlmutter, D.M. (1979) **Syntactic Argumentation and the Structure of English** Universsity of Califonia Press. Berkeley. Los Angeles. London.